

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

SIMU: MKURUGENZI WA MANISPAA

+ 255 736 200910

OFISI ZOTE: +255 736 200911/12

FAX: +255 028 736 200910

Barua pepe: md@ilemelamc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi,

Manispaa ya Ilemela,

S.L.P 735,

MWANZA.

Tovuti: www.ilemelamc.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela leo tarehe 27/02/2018 limepitisha makisio ya mpango na bajeti kiasi cha **Tsh. 68,613,400,00.00** kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha hizo Tshs. **15,013,332,000.00** ni ruzuku ya miradi ya maendeleo, **Tshs 1,620,686,000.00** ni ruzuku ya matumizi ya kawaida, Tshs. **42,75,317,000.00** mishahara, na **Tshs ,9024,065,000.00** ni mapato ya ndani.

Sambamba na uwasilishaji wa mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Halmashauri inawasilisha maombi maalum kwa serikali kuu yenye jumla ya **Tsh. 5,650,000,000/=** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Halmashauri, Ununuzi wa gari kwa ajili ya Idara ya Mipango Miji, fedha za malipo ya fidia ya wananchi waliotwaliwa maeneo yao kwa ajili ya matumzi ya Umma na fedha kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa Hospitali ya wilaya.

Ili kuongeza mapato ya ndani, halmashauri imejiwekea mikakati mbalimbali kuhakikisha kuwa mapato yanakusanywa kwa ufanisi ili kufikia malengo yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na ununuzi wa magari 3, uboreshaji wa miundombinu ya barabara kupitia wakala wa barabara (TARURA), kuboresha majengo ya kutolea huduma za afya na elimu. Halikadhalika imelenga kuboresha miundombinu ya mialo na masoko, pia kupitia kauli mbiu ya Wilaya "Ilemela ni yetu tushirikiane kuijenga", wannachi wataendelea kuhamasishwa juu ya uchangiaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wahisani na wadau wa maendeleo.

Vipaumbele vya miradi ya maendeleo vya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 katika sekta 11 ambazo ni Elimu, Ujenzi, Afya, Uwekezaji, Utawala, Maendeleo ya Jamii, Fedha na biashara, Uvuvi na Mifugo, Maji, Kilimo pamoja na Misitu/Nyuki.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya na kutumia kiasi cha Tshs 11,753,610,000.00 kutoka vyanzo vyake vya ndani. Kutokana na maelekezo ya serikali vyanzo vya mapato yatokanayo na kodi ya Majengo, mabango ya biashara na 30% ya kodi za Ardhi, vyanzo hivyo vilielekezwa kukusanywa na Serikali Kuu chini ya usimamizi wa mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA) jambo ambalo limepelekea bajeti ya Halmashauri kupungua kwa asilimia 23 ambayo ni sawa Tshs 2,729,545,000/= ya bajeti .Hata hivyo endapo vyanzo hivi vingekuwa chini ya Halmashauri bajeti ya mwaka 2018/2019 kwa upande wa mapato ya ndani makisio yangefikia Tshs 13,119,065,000.00 kwa ongezeko la Tshs 4,095,000,000.00 sawa na asilimia 17 ya bajeti ya sasa.

Imetolewa na:

Kitengo cha Teknolojia,Habari, Mawasiliano na Uhusiano
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela
27/02/2018